# KUSAMEHEWA NA MUNGU

GOSPEL 316

***"Heri mtu yule ambaye amesamehewa makosa yake, ambaye dhambi zake zimefunikwa."*** **Zaburi 32:1**

Makosa ambayo tunafanya (Kibiblia yanaitwa dhambi) hututenganisha na Mungu. Tunahitaji kusemehewa na Mungu ili tuwe na haki mbele Zake … na kuwa tayari kwa ajili ya milele. Msamaha wa Kibiblia haimaanishi kuwa Mungu atapuuza dhambi hizo na kufagilia mbali adhabu ya milele ya dhambi hizo. La! Hasha, adhabu hiyo lazima ilipiwe. Habari Njema (Injili) ni kwamba Yesu [Mungu-mwanadamu asiye na dhambi] alikwisha lipa adhabu hiyo kwa niapa yako na damu Yake kwa kufa msalabani. Kwa namna fulani alichukua nafasi yako. Yesu alikuwa dhabihu yako mbadala. Lakini hiyo haitoshi. Malipo hayo yanapaswa kutumika katika maisha yako … uhesabiwe. Swali muhimu ni, Je! hilo litafanyika kwa namna gani? Inafanyika wakati unatubu (kumrudia Mungu kutoka kwa dhambi zako) na kumwamini Yesu. Na hapo ndipo utakuwa umesamehewa na Mungu.

## *SHIDA YETU … UTENGANO*

*"kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."* Warumi 3:23

*"Dhambi zenu ndizo zinazowatenga na Mungu wenu, dhambi zenu zimemfanya ajifiche mbali nanyi hata asiweze kuwasikieni."* Isaya 59:2

*"Atawahukumu wale wasiomjua Mungu, wasioitii Habari Njema ya Bwana wetu Yesu. Wataadhibiwa kwa kuangamizwa milele na kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake."* 2 Wathesolonike 1:8-9

*"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."* Warumi 6:23

*"Tulipokuwa tungali wanyonge, wakati aliochagua Mungu, Kristo aliwafia wenye dhambi."* Warumi 5:6

## *SULUHU YA MUNGU … MBADALA*

*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."* Yohana 3:16

*"Na huu ndio upendo: si kwamba tulimpenda Mungu, bali yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili yeye awe dhabihu ya upatanisho* [dhabihu inayoridhisha] *kwa ajili ya dhambi zetu."* 1 Yohana 4:10

*"Lakini Mungu anaudhihirisha upendo wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu."* Warumi 5:8

*"Yeye mwenyewe alizibeba juu mtini dhambi zetu mwil ini mwake, ili tuwe wafu kwa mambo ya dhambi na tupate kuishi katika haki."* 1 Petro 2:24

*"Bali wote waliompokea,* [Yesu], *aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."* Yohana 1:12

## *NJIA YAKO YA MSAMAHA … NI KUMWAMINI YESU*

*"Manabii wote walishuhudia juu yake* [Yesu] *kwamba kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika Jina lake,"* Matendo 10:43. *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, si kwa matendo, ili mtu yeyote asije akajisifu,"* Waefeso 2:8-9. Unaweza kumwamini (na sio kuamini kuhusu) Yesu kwa kutubu … yaani kwa kumrudia Yesu kwa imani. Ombi ili ni njia mojawapo unaweza kufanya hivyo. Sio kiapo au tabano. Ikiwa hiyo ndio haja ya moyo wako, omba ombi hilo.

**Ee Mungu,**
**Ninaitikia haja yangu … mini ni mwenye dhambi.**
**Ninatubu … ninageukia kutoka dhambi ni zangu.**
**Ninamwamini Yesu … kwamba yeye kuwa Mungu, Alikufa msalabani kwa ajili yangu.**
**Ninamkaribisha Yeye awe Mwokozi wangu.**
**Amina**

Yesu alilipa adhabu ya dhambi zako. Na kwa kumwamini Yesu, malipo Yake yamekuwa malipo yako. Umesamehewa na Mungu. Na Yesu alisema kwamba umeokolewa kwa ajili ya milele, Yohana 3:16.

SWAHILI ***"Heri yake mtu aliyesamehewa kosa lake, mtu ambaye dhambi yake imeondolewa kabisa"*** **Zaburi 32:1**

Makala ya bure bila malipo ya *Kusamehewa na Mungu* katika lugha tofauti na yameunganishwa kutoka Gospel316.org.

**Ikiwa uliomba ombi hilo kwa kweli,** umesamehewa na Mungu na uko salama kwake milele yote. Kifo cha dhabihu cha Yesu kimekupa msamaha. Mungu ameahidi kwamba sasa una uzima wa milele kama miliki yako sasa … kwamba hautaingia hukumuni … na kwamba umeepuka kifo na kuingia katika uzima, Yohana 5:24. Sasa uko salama kwa kuwa hamna yeyote anaweza kukunyakua kutoka kwa mkono Wake wa nguvu. Anakushikilia kuliko vile unavyomshikilia Yeye. Yesu alisema, *"nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka mikono yangu. Baba yangu aliyenipa hawa ni mkuu kuliko wote na hakuna awezaye kuwapokonya kutoka mikononi mwake"* Yohana 10:28-29.

**Ikiwa hauko tayari kusema ombi hilo,** ifanye iwe kipaumbele chako cha juu. Uamuzi wako ni wa manufaa ya milele au madhara ya milele. Hamna nafasi nyingine kaburini, *"Na kama ambavyo mwanadamu ameandikiwa kufa mara moja tu, na baada ya hapo kukabili hukumu,"* Waebrania 9:27. Ikiwa una maswali ambayo hauna jibu na hiyo inakuzuia kufanya uamuzi, zungumza na mtu ambaye alikupa nakala hii.

## Vielezo na Ufafanuzi

**Msamaha.**
Msamaha. Msamaha wa Kibiblia unahitaji malipo ya adhabu ya dhambi zetu. Adhabu ya dhambi ni utengano na Mungu milele. Msamaha wa Kibiblia ni uhamisho wa dhambi zako na adhabu yake kutoka kwako hadi kwa Yesu. Mungu alimutwika Yesu asiye na dhambi dhambi zetu na adhabu yake. Ndipo Mungu akatupa haki yake. Ni kana kwamba kulikuwa na vitabu viwili mbinguni. Kitabu cha kwanza, ni kitabu cha matendo yako, kina alama ndani yake kwa kila kosa ambalo umewahi fanya. Kurasa zake zimejaa na alama za makosa. Biblia inasema wazi kwamba mambo mengine tunayofanya ni dhambi (dhambi ya makusudi) na mambo mengine tunayofanya ni dhambi (dhambi isiyotarajiwa). Hata baadhi ya mawazo yanaweza kuwa maovu. Dhambi mara tatu kwa siku ni sawia na 1,000 kila mwaka. Katika maisha hizo ni dhambi nyingi sana. Kitabu kingine ni kitabu kitakatifu cha Yesu. Kurasa zake ni safi na hazina lawama. Wakati unamwamini Yesu, ni kana kwamba Kurasa za vitabu hivyo viwili vinabadilishwa. Kisha kitabu cha kumbukumbu kilicho na jina lako kinakuwa safi kabisa. Dhambi yako na adhabu yake imefutiliwa mbali.

**Suluhisho la kweli.**
Yesu akawaambia, *"Mimi ndiye Njia na Kweli na Uzima; mtu hawezi kufika kwa Baba bila kupitia kwangu,"* Yohana 14:6. Suluhu ya Biblia kwa dhambi zetu ambazo zilizababisha utengano wetu na Mungu ni za kipekee. Dini zingine zinatuhitaji tukabili umelele na dhambi zetu kwa matumaini kwamba Mungu yeyote ambaye anaweza kuwa huko hatazitilia maanani. Njia ya Yesu ni ya ajabu kwamba inasamehe dhambi zetu … inatusafisha na kuwa wasafi. Kisha tunakutana milele na Mungu huku dhambi zetu zikiwa zimefutwa kwa sababu zilitunikwa kwa Yesu. Mtume Petro alisema, *"Wokovu unapatikana kwake tu; kwa maana hakuna jina jingine duniani ambalo wamepewa wanadamu kuwaokoa ila jina la Yesu, na ni kwa jina hilo peke yake tunaweza kuokolewa,"* Matendo 4:12. Mtume Paulo aliandika *"Maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani mwanadamu Kristo Yesu, aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote. Yeye ni uthibitisho wa mambo haya, uliotolewa kwa wakati wake,"* 1 Timotheo 2:5-6. Njia ya Yesu ndio suluhisho la kweli.

**Kumwamini Yesu.**
Kumwamini Yesu ni zaidi ya *kuamini kuhusu* Yesu. Hebu fikiria kwamba uko katika ndege kama msafiri ukiwa angani juu ya milima kwa ghafla injini inaanza kurupuka na kukosa kufanya kazi. Ndege inaanza kushuka ikielekea kuanguka. Rubani anaamrisha kila mtu kujifunga mwavuli wa kupepea na kuondoka kwa ndege kupitia mlango uliofunguliwa. Ushajua kuhusu mwavuli (parachuti). Umeziona katika runinga. Lakini sasa hali ni tofauti. Kuondoka ndani ya ndege kupitia mlango ulio wazi kunahitaji zaidi ya *kuamini kuhusu* parachuti … inahitaji *kuiamini* parachuti. Na mkoba wa mtembeaji wa masafa marefu hautasaidia. Kuponea kwako kunahitaji parachuti sahihi … ukiondoka nje bila parachuti ni kifo kwa hakika. Ukiondoka nje ya ndege ukiwa na parachuti ni imani asili mia moja (100%). Unaweza kuwa na shaka … lakini kuponea kunahitaji imani kamili katika parachuti. Yesu ndiye parachuti ya kweli. Tembea kwa imani. Mwamini Yeye!

**Kuchapisha maagizo.** Uchapishaji wa pande mbili katika ukurasa mmoja unapendekezwa. Unaweza kuchapisha kwa rangi au rangi nyeusi/nyeupe.

---

*Kusamehewa na Mungu* © 2024 imechapishwa na Acts One Eight na inatoka www.Gospel316.org. Uko na uhuru wa kutoa nakala yako, au kuituma bila kubadilisha huku kanuni zake zote zikiwemo. Ijapokuwa, unaweza kuongezea huduma yako au jina la kanisa yako au nembo. Acts One Eight inaangazia Biblia peke yake. Ipo ili isaidie watu kuja katika imani katika Kristo Yesu na kukua na kuwa wanafunzi wake. Tafsiri zisizo za Kiingereza zinatolewa na www.ChristianLingua.com. nukuu za Biblia katika makala maalumu zinatoka katika toleo la New American Standard Bible (NASB). Nukuu za Biblia katika toleo hili zinatoka katika "Biblia Neno Takatifu".